**BENKI YA MAENDELEO YA KILIMO TANZANIA**

TADB
"Benki ya Wakulima"

10 Years
Muongo Mmoja wa Mabadiliko

# NANENANE

## 2025, DODOMA

# NA MIAKA 10 YA TADB






“Nitumie fursa hii kushukuru wadhamini wa Maonesho haya ya Nanenane. Lakini nashukuru sana mdhamini mkuu ambaye ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo, TADB na naipongeza kwa kutimia miaka 10 ya ukuaji wa haraka.

Benki hii ina miaka 10, lakini ndani ya kipindi cha miaka minne TADB imeonesha kukua kwa haraka sana; Hongereni sana! Wamekua kwa kiasi cha kudhamini maonesho haya, Hongereni sana.”

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania




#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation

TADB
"Benki ya Wakulima"

Kongole TADB kwa kuleta

# Mageuzi Makubwa

kwenye sekta ya Kilimo




Years
Muongo Mmoja wa Mabadiliko

# YALIYOJIRI WAKATI BENKI YA MAENDELEO YA KILIMO (TADB) IKIKABIDHI HUNDI YA MFANO KAMA MDHAMINI MKUU WA MAONESHO YA NANENANE KITAIFA YALIYOFANYIKA JIJINI DODOMA KUANZIA AGOSTI 1 - 8, 2025

Dodoma






## ALIYOSEMA KATIBU MKUU WIZARA YA KILIMO BW. JERALD MWELI

# Benki ya Maendeleo ya Kilimo ni Mdhamini Mkuu wa Maonesho ya Nanenane Kitaifa kwa kuchangia shilingi milioni 400 za Kitanzania.

# Nanenane ya mwaka huu itaenda sambamba na maadhimisho ya miaka 10 ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB)

# Benki ya Maendeleo ya Kilimo imechagiza mageuzi makubwa katika Sekta ya Kilimo kupitia mikopo iliyotoa kwa wakulima.

# Wakati wa Maonesho ya mwaka huu 2025, kutakuwa na shughuli mbalimbali ikiwemo makongamano, huduma kutoka taasisi za kifedha kwa wakulima na elimu kwa wakulima itatolewa hapa.

# Benki ya Maendeleo ya Kilimo imetoa mikopo ya zana za kilimo na pembejeo za kilimo kwa wakulima wetu ili kukuza Sekta ya Kilimo.

## MKURUGENZI MTENDAJI WA BENKI YA MAENDELEO YA KILIMO TANZANIA (TADB) BW.FRANK NYABUNDEGE

# Utashi wa Kisiasa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan umewezesha Benki hii kuwa miongoni mwa benki kubwa hapa nchini.

# Sekta ya kilimo imeajiri zaidi ya asilimia 70 ya watanzania, hivyo ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi.

# Benki ya Maendeleo ya Kilimo ni Kinara katika utoaji wa mikopo katika sekta ya kilimo kwa lengo la kuwawezesha wakulima kuongeza tija.

# TADB inashirikiana na benki 19 katika kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima kwa dhamira ya kukuza sekta ya kilimo.

# Ukubwa wa benki kwa sasa una thamani ya shlingi trilioni 1.2 kutokana na uwekezaji uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita tangu ilipoingia madarakani mwaka 2021.

# Mikopo iliyotolewa na Taasisi za fedha kwa sekta ya kilimo imefikia zaidi ya shilingi trilioni 4 katika kipindi cha Rais Samia Suluhu Hassan.

# Kumekuwa na ushirikiano mzuri kati ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Wizara za Kisekta.

# TADB inashirikiana na Benki 19 kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima hapa nchini kwa dhamira ya kukuza Sekta ya Kilimo.

*Imeandaliwa na **Idara ya Habari Maelezo***




SIKU YA 1

# TADB yachagiza Mageuzi Makubwa Sekta ya Kilimo Nchini

Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, akoshwa na vikundi mbalimbali vikishuhudia kunufaika na mikopo wezeshi kutoka Benki ya Kilimo, TADB.

Dodoma

Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuleta mapinduzi ya kilimo kwa vitendo kupitia mikopo yenye riba nafuu na uwezeshaji wa wakulima wadogo na wa kati kupitia TADB.

Hayo yalisemwa Agosti 1, 2025 katika viwanja vya NaneNane jijini Dodoma na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) Bw.Frank Nyabundege wakati akitoa maelezo kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango alipotembelea banda la Benki hiyo kabla ya kufungua maonesho hayo Kitaifa.

“Zaidi ya wakulima **milioni 1.95** wamefikia ndoto zao kupitia TADB, huku zaidi ya shilingi **trilioni 1.13** zikitolewa tangu 2015 kama mtaji wa mabadiliko kwa kilimo cha Tanzania”, alisisitiza Nyabundege

Akifafanua Bw. Nyabundege amesema TADB si tu Benki ni nguzo ya matumaini, injini ya uzalishaji, na daraja la maendeleo kwa wakulima wa Tanzania.

Aidha, Benki hiyo ni mdhamini mkuu wa maonesho ya NaneNane Kitaifa yaliyofunguliwa leo Agosti 1, 2025 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani Mhe. Dkt Philip Mpango.

Sambamba na Maonesho hayo, TADB inasherekea miaka 10 ya mafanikio tangu kuanzishwa kwake. Benki hiyo kwa sasa ni miongoni mwa benki kubwa nchini na imewezesha sekta ya kilimo kutoa mchango mkubwa katika ujenzi wa Taifa.

### Dkt. Mpango Aipongeza TADB

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango ameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kuwezesha wakulima kujikwamua kiuchumi kupitia mikopo yenye riba nafuu.

Aliyasema hayo Agosti 1, 2025 jijini Dodoma katika viwanja vya Nane Nane alipotembelea Banda la TADB kabla ya kufungua rasmi maonesho hayo Kitaifa.

“Nawapongeza TADB na ninawaelekeza kuendelea kuwafikia watanzania wengi zaidi kwa ajili maendeleo endelevu ya nchi yetu, “ alisisitiza Dkt. Mpango.

Akizungumza namna Benki hiyo inavyokuza uchumi amesema imewezesha vijana na akina mama kujiajiri kwa kupatiwa zana za kilimo zenye ubora na zenye kuleta tija.

Maonesho ya NaneNane Kitaifa yanafanyika katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma Kitaifa na yamefunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


## Mapinduzi ya Kiuchumi

Wanufaika

**1,953,162**

Wakulima wamefikiwa kutoka katika nyanja mbalimbali za kiuchumi kote nchini.


Shilingi trilioni **1.13** zatolewa tangu 2015




#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation

SIKU YA 2

# TADB Yafanya Mafunzo Kwa Vijana wa BBT - Chinangali Dodoma






*#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation*

## Vijana wa BBT - Chinangali Dodoma wakifuatilia mafunzo yaliyokuwa yakitolewa na Maafisa wa TADB




Kuelekea maadhimisho ya miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuwawezesha wakulima na vijana kupitia mafunzo ya kiujuzi na kifedha.

Tarehe 2 Agosti 2025, TADB imeendesha mafunzo kwa vijana 96 waliopo katika Mpango wa Building a Better Tomorrow (BBT), ikiwa ni sehemu ya juhudi zake za kuwawezesha vijana kujikita kikamilifu kwenye sekta ya kilimo. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo katika maeneo muhimu kama vile elimu ya fedha, uwekezaji, bima za kilimo, na maadili.

Katika kufanikisha mafunzo haya, TADB imeshirikiana na taasisi washirika zikiwemo Shirika la Taifa la Bima (NIC), Mfuko wa Pamoja wa Uwekezaji (UTT), na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Kupitia ushirikiano huu, benki inaendelea kuonesha dhamira yake ya dhati ya kuchagiza maendeleo ya kilimo na kuwaandaa vijana kuwa wakulima wa kisasa, wenye maarifa na uwezo wa kushindana kwenye soko la kisasa la kilimo.

Kwa upande mwingine;

## KATIBU TAWALA MKOA WA SINGIDA ATEMBELEA BANDA LA TADB

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dkt. Fatuma Ramadhan Mganga, ambaye pia ni **Mgeni Rasmi katika siku ya pili ya Maadhimisho ya Nane Nane** tarehe 2 Agosti 2025, ametembelea banda la Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), mdhamini mkuu wa maonesho hayo, na kujionea shughuli mbalimbali za benki hiyo pamoja na kuzungumza na baadhi ya wanufaika wa mikopo ya TADB.

Dkt. Fatuma ameipongeza TADB kwa mafanikio makubwa iliyoyapata katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, hususani katika kuchagiza maendeleo ya kilimo nchini. Aidha, ametoa wito kwa Benki hiyo kuongeza jitihada katika kuhakikisha Mkoa wa Singida na maeneo mengine ya Kanda ya Kati yanapata visima vya maji vya kutosha kwa ajili ya Kilimo cha umwagiliaji.

TADB imemshukuru Dkt. Fatuma kwa kutambua mchango wake katika Sekta ya Kilimo, na kuahidi kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha upatikanaji wa visima vya maji katika Kanda ya Kati kwa ajili ya kuendeleza skimu za umwagiliaji.



SIKU YA 3

Dodoma

# Waziri Mkuu Aipongeza TADB kwa Kuleta Mageuzi ya Uvuvi Tanzania

Waziri Mkuu  wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kuleta mageuzi makubwa ya Kilimo nchini.

Amesema hayo leo tarehe 3 Agusti, 2025 mara baada ya kutembelea banda la Mdhamini Mkuu wa Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima maarufu kama Nanenane ambaye ni TADB.

"Ninawapongeza TADB kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuchagiza maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Ufugaji kwani ndiyo uti wa mgongo wa taifa letu na imeajiri zaidi ya asilimia 65 ya wananchi," alisisitiza Mhe. Majaliwa

Akitoa maelezo kwa Waziri Mkuu kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji  wa TADB, Mkurugenzi wa Mipango, Ushauri na Mahusiano ya Taasisi Bwana Mkani Waziri alisema  kuelekea kilele cha maadhimisho ya miaka kumi ya TADB tangu kuanzishwa kwake 2015, Benki hiyo imepata mafanikio mengi, ikiwa ni pamoja na ukuaji benki toka benki ndogo hadi kufikia benki kubwa katika utoaji wa huduma za kifedha nchini.

"Benki ilianza na mtaji wa bilioni 60, lakini hivi leo benki imetoa mikopo yenye  thamani ya tirilioni 1.129 ambayo ni mafanikio makubwa yanayotokana na utashi wa Serikali  wa Awamu ya Sita iliyowekeza kwenye Sekta ya Kilimo na Mifugo kwa ajili ya kuwakomboa wakulima ambao walikuwa hawapati fursa ya mikopo yenye riba ndogo awali" amesema Mkani.

Maonesho ya Wakulima ya Nanenane yanaenda sambamba na kaulimbiu inayosema " Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi 2025.





#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation

SIKU YA 4

Dodoma

# TADB yafadhili na kushiriki Mdahalo wa Vijana kuhusu Hatma ya Kilimo kwenye Miaka ijayo






Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imeshiriki katika mdahalo wa vijana uliofanyika kwenye ukumbi wa Nane Nane Grounds, Dodoma, kujadili mustakabali wa kilimo kwa miaka 10 ijayo.

Katika mdahalo huo, TADB iliwakilishwa na Mtaalamu wake Ndugu Richard Sempindu, ambaye alishirikiana na wachangiaji wengine akiwemo Dkt. Eliaza kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe na Mr Daudi Manongi kutoka Tanzania Alliance for Biodiversity. Wote walichangia kwa kuchochea mijadala na kutoa majawabu kuhusu mwelekeo wa kilimo na vijana nchini katika miaka ijayo.

Mdahalo huu ulihudhuriwa na vijana zaidi ya 50 wenye maono ya kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo.

TADB imeshirikiana na taasisi ya Shamba Box kufanikisha tukio hili muhimu.

*#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation*

SIKU YA 5

Dodoma

# KUELEKEA **MIAKA 10 YA TADB**

## Benki ya Maendeleo ya Kilimo imeendelea kuwawezesha wakulima kwa kuwajengea uwezo wa kitaalamu.



Agosti 5,2025, ilikuwa zamu ya wakulima 95 kutoka mikoa ya Singida na Dodoma, wanaojihusisha na kilimo cha zabibu na korosho.

Mafunzo haya yaligusa maeneo muhimu kama vile uwekezaji, bima, maadili na elimu ya fedha, na yaliendeshwa na wataalamu kutoka TADB kwa kushirikiana na maafisa kutoka NIC, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na UTT-AMIS



Kwingineko Visiwani Zanzibar;

## TADB Yawezesha Mapinduzi ya Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Visiwani Zanzibar

Upatikanaji wa huduma za Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) visiwani Zanzibar umefungua fursa mpya za kiuchumi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi kupitia mikopo nafuu, elimu ya fedha na uhusiano wa moja kwa moja na masoko ya uhakika.

Hayo yamesemwa na Meneja wa TADB Kanda ya ZANZIBAR Ally Singoi, Agosti 5, 2025 katika maeonesho ya Nane Nane visiwani Zanzibar wakati wa mahojiano maalumu kuhusu utekelezaji wa Benki hiyo kwa upande wa Zanzibar.

"TADB imewezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo kilimo cha umwagiliaji, ufugaji wa kisasa, uvuvi endelevu, usindikaji wa mazao ya kilimo, biashara ndogondogo zinazoendeshwa na vijana na wanawake kwenye mnyororo wa thamani ya Sekta za kilimo, mifugo na uvuvi", alisisitiza Singoi

"Hadi sasa jumla ya miradi 43 imenufaika moja kwa moja na huduma hizi, ikiwemo miradi 7 inayomilikiwa na wanawake na miradi 4 ikiwa ni vijana . Sanjari na hayo jumla ya miradi10 imefadhiriwa ikiwa inamilikiwa na vyama vya ushirika (8 kutoka Pemba na 2 kutoka Unguja). Miradi yote hii imeunganishwa katika mifumo rasmi ya kibenki na masoko," alisisitiza Singoi

TADB Kanda Zanzibar imewezesha miradi inayohusisha uzalishaji wa mazao ya biashara kama karafuu, ufugaji wa kuku wa mayai, uvuvi wa samaki kwa vizimba, pamoja na kilimo mseto kinachowahusisha vijana na wanawake. Aidha, benki imekuwa ikitoa mafunzo ya kilimo biashara na ujasiriamali kwa wakulima wapya jambo lililowasaidia kubadili mtazamo kutoka kilimo cha kujikimu hadi kilimo chenye tija.






Mpaka sasa kwa mijibu wa Singoi zaidi ya wanufaika 200 wameshafikiwa kupitia mradi huu ambapo jumla ya ng'ombe wa maziwa (Improved heifers) 352 wenye thamani ya shilingi 993,294,050 wametolewa vilevile wafugaji hao waliopatiwa mikopo wamepewa ruzuku fungamanifu zenye thamani ya TZS 222,000,000 ili kuwapunguzia mzigo wa ulipaji mikopo ili kuongeza tija na uzalishaji.

Pia, kwa kushirikiana na Idara ya Mifugo Zanzibar na Shirika la Heifer International, Mradi huu pia umewezesha elimu ya ufugaji bora, uhimilishaji wa kisasa, upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, lishe bora, na uwezeshaji wa vifaa kama pikipiki za maafisa ugani, mashine za kukatia majani, vifaa vya tiba, kompyuta na miundombinu ya ukusanyaji maziwa, jumla ya wafugaji 1583 (wanawake 453) wamefikiwa.

Mipango ya sasa inahusisha uwezeshaji wa miradi ya kilimo cha baharini kama vile ufugaji wa majongoo bahari, na usindikaji wa mazao ya kilimo unaofanywa na wanawake na vijana.

Benki imeidhinisha fedha kiasi cha bilioni 22 kwa ajili ya mwaka huu wa 2025, bilioni 16 zikienda kwenye karafuu, bilioni 3.8 zikienda kwenye wafugaji wa kuku, wafugaji wa ng'ombe wa maziwa bilioni 1.1 , wakulima wa mboga mboga 1.2.




#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation

SIKU YA 6

Dodoma

# KUELEKEA **MIAKA 10 YA TADB**

TADB imeendelea kutoa elimu ya kitaalamu kwa Wakulima na Wafugaji ili kuwaongezea ujuzi na uwezo.



Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imeendelea kutoa elimu ya kitaalamu kwa wakulima ili kuwaongezea ujuzi na uwezo. Katika siku ya sita ya maonesho, wakulima 98 wa zabibu kutoka vijiji vya Hombolo na Andali, vilivyopo Chamwino na Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma Mjini, walipata nafasi ya kushiriki mafunzo ili kuongeza tija katika kilimo chao.

Mafunzo haya yalijikita katika maeneo muhimu ikiwemo elimu ya uwekezaji, bima, maadili na fedha, yakifundishwa na wataalamu kutoka TADB kwa kushirikiana na Maafisa kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na UTT-AMIS.






*#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation*

Wakati huo huo;

## KATIBU MKUU, WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI ATEMBELEA BANDA LA TADB.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Ally Senga Gugu, ametembelea banda la maonesho la Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na Benki pamoja na mafanikio ya wanufaika wa mikopo yake.

Katika ziara hiyo, Mhe. Gugu ameipongeza TADB kwa mchango mkubwa inaoutoa katika kuwawezesha wakulima wadogo na wa kati, ambao ni nguzo muhimu ya maendeleo ya taifa kupitia sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi. Amehimiza pia umuhimu wa Benki kuendelea kupanua wigo wa huduma zake kwa kufungua ofisi katika maeneo mengi zaidi nchini, ili kuwafikia wakulima walio mbali na ofisi zilizopo sasa.

Kwa upande wa TADB, Mkurugenzi wa Mipango, Ushauri na Mahusiano ya Taasisi, Bw. Mkani Waziri, amemshukuru Mhe. Gugu kwa maoni yake na kuthibitisha kuwa Benki imeupokea ushauri huo kwa uzito na itaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha huduma zake zinawafikia wakulima wengi zaidi nchini.



# Nane Nane Zanzibar

Mkurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania, Zanzibar, Bw. Ibrahim Malogoi, ametembelea banda la TADB katika Maonesho ya Nanenane Zanzibar na kupata maelezo kuhusu huduma za TADB, hususan namna inavyowezesha wakulima, wafugaji na wavuvi visiwani.

Meneja wa TADB Kanda ya Zanzibar, Bw. Ally Jamal, ameeleza utekelezaji wa miradi na mipango ya benki, ikiwemo mikopo ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Bw. Malogoi ameipongeza TADB kwa kutimiza miaka 10 ya kuendeleza sekta ya kilimo na kuahidi ushirikiano wa karibu, akisisitiza kuwa ofisi yake iko wazi muda wote.




# Ushirikiano kwa maendeleo ya Uchumi wa Buluu Zanzibar!

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Captain Hamad Bakar Hamad, ametembelea banda la TADB katika Maonesho ya Nane Nane Zanzibar yanayoendelea kwenye Viwanja vya Dole Kizimbani, Unguja.

Katika banda hilo, amepokelewa na Meneja wa Kanda, Bw. Ally Jamal, pamoja na wafanyakazi wa TADB, Katibu Mkuu amepatiwa muhtasari wa maendeleo ya benki, hususan katika utoaji wa mikopo kwa wakulima wadogo, wa kati, na wakubwa kwenye minyororo ya thamani ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

Katika mazungumzo hayo, wamejadili fursa zinazopatikana kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na namna ya kushirikiana kuzifikia, ikiwemo utekelezaji wa miradi ya kimkakati itakayochochea mapinduzi ya uchumi wa buluu Zanzibar.




*#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation*

SIKU YA 7

Dodoma

# WAZIRI MKUU MSTAAFU **MHE. MIZENGO PINDA ATEMBELEA BANDA LA TADB**

Waziri Mkuu Mstaafu, Mhe. Mizengo Pinda, ametembelea banda la maonesho la Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) katika viwanja vya Nane Nane, Nzuguni – Dodoma, na kujionea mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 ya utekelezaji wa majukumu ya Benki hiyo.

Katika mazungumzo yake, Mhe. Pinda ametoa pongezi kwa TADB kwa mchango wake katika kuendeleza sekta ya kilimo, huku akisisitiza umuhimu wa kuimarisha juhudi za kuwawezesha wanawake zaidi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kilimo na kuongeza uzalishaji.



WAKATI HUOHUO;

# WAZIRI WA KILIMO, **MHE. HUSSEIN BASHE NAYE ALITEMBELEA BANDA LA TADB**



Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, ametembelea banda la maonesho la Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) katika viwanja vya Nane Nane, Nzuguni – Dodoma, ambapo amejionea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 ya utekelezaji wa majukumu ya Benki hiyo.

Aidha, amepata fursa ya kuzungumza na baadhi ya wanufaika wa mikopo ya TADB waliopo kwenye maonesho hayo, na kusikiliza ushuhuda wao kuhusu mchango wa TADB katika kuboresha shughuli zao za kilimo.

SIKU YA 8

Dodoma

# SIKU YA NANENANE

## Rais Samia Aipa Kongole **Benki ya Wakulima** kwa Utendaji Bora












Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa utendaji mzuri ulioleta tija kwa wakulima.

Aliyasema hayo Agosti 8, 2025 wakati akihutubia wananchi katika kilele cha **Maadhimisho ya Nane Nane** Kitaifa katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Rais Samia alisema utendaji mzuri wa Benki hiyo umeipa uwezo wa kuwezesha wananchi na kuendelea kuwa mdhamini mkuu wa maonesho hayo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Maadhimsho ya Nane Nane Kitaifa yamefanyika Dodoma na yameshirikisha wakulima, wafugaji na wavuvi kutoka katika mikoa mbalimbali nchini.

*#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation*

# Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla **ameipongeza Benki ya TADB**



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, ambaye pia alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya kufunga Maonesho ya Kilimo (Nane Nane) Zanzibar, ameipongeza Benki ya TADB kwa mchango wake mkubwa katika kuendeleza sekta ya kilimo na kuchochea ukuaji wa uchumi wa visiwani. Pia, Mhe. Hemed aliitambua TADB kama mdhamini wa maonesho hayo, akisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa wadau katika kuinua sekta ya kilimo - tarehe 14/08/2025.

Katika banda la TADB Mhe. Hemed Suleiman Abdulla amepokelewa Meneja wa Kanda ya Zanzibar, Bw. Ally Jamal na kupatiwa muhtasari wa maendeleo ya benki ikiwemo taarifa ya utolewaji wa mikopo, idadi ya wanufaika wa mikopo ya benki Zanzibar pamoja na:

Maendeleo ya Mfuko wa Dhamana wa Wakulima Wadogo (SCGS) na namna unavyofanyakazi kwa kushirikiana na mebenki ya kibiashara na taasisi za kifedha katika kutoa mikopo kwa makundi ya wakulima wadogo, wa kati na wakubwa katika minyoro ya thamani ya kilimo, ufugaji na uvuvi Pamoja na Mradi Shirikishi wa Wasindikaji na Wazalishaji wa Maziwa Tanzania (TI3P).

Katika hotuba yake ya kufunga maonesho, Mhe. Hemed ametoa rai kwa vijana na kuwahimiza kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kilimo na kuachana na tabia hatarishi, ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya na mienendo mingine inayorudisha maendeleo nyuma.



Dodoma

Ikitimiza **Miaka 10** tangu kuanzishwa kwake

# **Benki ya Wakulima (TADB)** yafanya hafla ya kukata Keki na kuwaenzi Maafisa waliostaafu













#KilimoKinaBenkika #UvuviNiUtajiri #MifugoNiUtajiri #Nanenane2025 #aDecadeOfTransformation

# The Team ...




# NANENANE

**2025, DODOMA**




10 Years
Muongo Mmoja wa Mabadiliko




TADB
"Benki ya Wakulima"

10 Years
Muongo Mmoja wa Mabadiliko

**Benki ya Maendeleo ya Wakulima Tanzania**
Orofa ya 4, Jengo la ACACIA, Kitalu Na. 84-14109 Kinondoni, Barabara ya Kinondoni
S.L.P 63372, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 292 3500 | Namba (Bure): 0800 110 120 | Baruapepe: info@tadb.co.tz

## Ofisi za Kanda

**Kanda ya Kati**
Jengo la Mkandarasi, Kitalu Na. 5, Eneo NCC,
Mtaa wa Tambukareli
S.L.P 2143, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 26 296 3849
Baruapepe: dodoma@tadb.co.tz

**Kanda ya Kusini**
Jengo la RAHA LEO,
S.L.P 331, Mtwara, Tanzania.
Simu: +255 23 293 5632
Baruapepe: mtwara@tadb.co.tz

**Kanda ya Mashariki**
Kitalu Na. 102,
Barabara ya Kinondoni
S.L.P 75835, Dar es Salaam, Tanzania.
Baruapepe: dar@tadb.co.tz

**Kanda ya Kaskazini**
Orofa ya Chini, Jengo la PSSSF, Kitalu Na. 15,
Barabara ya Nyerere
S.L.P 16965, Arusha, Tanzania.
Simu: +255 27 297 1075
Baruapepe: arusha@tadb.co.tz

**Nyanda za Juu Kusini**
Jengo la NHC, Kitalu Na. 20, Mtaa wa Jacaranda,
S.L.P 2581, Mbeya, Tanzania.
Simu: +255 25 250 3053
Baruapepe: mbeya@tadb.co.tz

**Kanda ya Ziwa**
Jengo la TBA (Zamani, Ofisi za TRA),
Barabara ya Ofisi za Posta
S.L.P 141, Mwanza, Tanzania.
Simu: +255 28 254 1763
Baruapepe: mwanza@tadb.co.tz

**Kanda ya Magharibi**
Kitalu Na. 36,
Jengo la Kalunde,
Barabara ya Kitete,
S.L.P 1025, Tabora, Tanzania.
Baruapepe: tabora@tadb.co.tz

**Kanda ya Zanzibar**
ZURA Makao Makuu,
Orofa ya Chini,
Mtaa wa Maisara,
P.O.Box 291, Zanzibar.
Simu (Bure): 0800 110 120